

# **MCHANGO WA MATAMBIKO YA KIFO KATIKA KUHFADHI FASIHI SIMULIZI, KIFANI CHA JAMII YA WALUO: MIGORI.**

OWALA, J.A. (PhD)

**Chuo Kikuu Cha Rongo**

**Kitivo Cha Elimu Na Sayansi Ya Jamii**

**Idara Ya Lugha, Isimu Na Fasihi**

**[Jaelowala@gmail.com](mailto:Jaelowala@gmail.com)**

## **IKISIRI**

*Matambiko yalianza zamani sanakatika enzi za mababu zetu. Matambiko yenyewe yalinuia mwanadamu kutafuta suluhu ya mambo ambayo kwa uwazi yalikuwa nje ya uwezo wao kama vile kifo. Yalifanywa ili kuomba msaada kwa Mungu ili kupata nafuu juu ya shida husika. Utaratibu huu ukarithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Katika jamii nyingi za Kiafrika, matambiko bado yanachukuliwa kuwa na umuhimu mkubwa sana. Waluo kwa mfano, ni kabila kutoka Sudan Kusini wanaopatikana Kenya, Uganda na Tanzania. Ni mkusanyiko wa kabila la kinailoti ambalo lilisafiri kutoka Afrika ya Kaskazini kufuata mto Nile kuja Kusini. Wengi wao wameenea kando kando ya Ziwa Viktoria. Nchini Kenya, Waluo wanajulikana kama kabila ambalo limeipa kipau mbele mahali pao pa mazishi. Wanajulikana kufanya matambiko zaidi ya kumi wakati wa kifo. Lengo kuu la utafiti huu ni kubaini mchango wa matambiko ya kifo katika fasihi simulizi. Utafiti utahusu jamii ya Waluo wanaoishi katika kata ndogo ya Suna Magharibi, katika Kaunti ya Migori. Maswali yatakayojibiwa ni; Je, maigizo ni yapi katika matambiko yale ya kifo? Je, maigizo yale yana nafasi gani katika fasihi simulizi kwa jumla? Nadharia itakayotumiwa ni nadharia ya sosholojia ya Auguste Comte. Mbinu ambazo zitatumwa ni za mahojiano na uchunguzi ushiriki.*